

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

TARHIE: 31/05/2022

**TANGAZO**  
**LA**  
**KUTOA HUDUMA YA ULINZI**  
**LGA/121/2022/2023/NC/01**


1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inapenda kuwatangazia wananchi wote wenye Makampuru ya Ulinzi yenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya ulinzi katika Ofisi na maeneo mbalimbali yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Kazi hii ni kuanzia tarehe 01 Julai, 2022 hadi tarehe 30 Juni, 2023
2. Unakaribishwa kuleta Vidadisi bei vyako vya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyotatanuliwa katika Sehemu ya II
3. Vitabu vya Vidadisi bei vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 15,000/ kwa Kampuni itakayomba kazi hii

Vidadisi bei vyote vitumwe vikiwa vimejazwa nakala halisi (ORIGINAL - MOJA) na (COPY - MBILI) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha na juu yake iandikwe kama ifuatavyo.

**"KIDADISI BEI NA. LGA/121/2022 - 2023 /NC/01" KWA UTOAJI WA HUDUMA YA ULINZI KATIKA OFISI NA MAENEO MBALI MBALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

4. Maombi vote yapelekwe (yatumwe) kwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Kitengo cha Manunuzi, S..L.P 70, SIKONGE.
5. Kampuni iwe na Walinzi waliopitia mafunzo ya Mgambo au JKT na wawe waaminifu kulinda mali za umma

- 6 Kampuni iwe na Dhamana ya MALI ISIYOHAMISHIKA kama Bondi ya Benki nk. Kwa ajili ya kulipa fidia pindi wizi au uharibifu wowote utatokea wakati wa kutekeleza mkataba
- 7 Kampuni iwe na Leseni halali ya Biashara na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
- 8 Kampuni ionyeshe utambulisho kwamba inalipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
- 9 Kampuni iwe imesajiliwa na Msajili wa Makampuni (Brela) na kivuli cha usajili kiambatanishwe kwenye maombi yake
- 10 Kampuni ionyeshe gharama ya Mlinzi mwenye silaha (Armed security Guard) na gharama ya mlinzi asiyekuwa na silaha (Anarmed security Guard).
- 11 Siku ya mwisho ya kuwasilisha Nukuu za bei ni siku ya Jumatatu tarehe 13.6.2022 saa 5:00 Asubuhi. Nukuu za bei zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari
- 12 Nukuu za bei zitakazochelewa, sehemu ya nukuu ya bei, nukuu za bei za kielektroniki, na nukuu za bei zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji wa nukuu za bei, kwa hali yoyote ile nukuu za bei hizo hazitakubaliwa kwa tathmini

  
Seleman M. Pandawe

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
SIKONGE**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HAYYA - SIKONGE**